LEGAL AND HUMAN RIGHTS CENTRE

LHRC

KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU

KIJARIDA KUHUSU

# SHERIA YA KUINGILIA KITU KISICHOKUWA CHA KWAKO

*Kwa Jamii yenye Haki na Usawa*




## Unaweza kutoa taarifa za ukiukwaji wa haki kupitia

# #HakiKiganjani

SMS **0699695486**

Pakua AnroidApp ya **Haki Kiganjani**

hakikiganjani.humanrights.or.tz

***Usipotezee, toa taarifa sasa!***

KIJARIDA KUHUSU

# SHERIA YA KUINGILIA KITU KISICHOKUWA CHA KWAKO

**Kimeandaliwa na:**

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu

# YALIYOMO

**SHUKRANI** ........................................ **5**

**DIBAJI** ........................................ **6**

**MAONO** ........................................ **8**

**1. Maana ya Kuingilia Kitu Kisichokuwa Chako** ........................................ **9**

**2. Aina za Kuingilia Kitu Kisichokuwa Chako** ........................................ **9**

2.1.Kumuingilia/kumbughudhi Mtu bila Idhini Yake ........................................ 9

2.2.Kushambulia kwa Kumtupia Mtu kitu au Kushambulia kwa Maneno ........................................ 10

2.3.Kutumia nguvu kwa Makusudi kwa Lengo la Kuumiza ........................................ 10

2.4.Kumfunga Mtu Akashindwa Kufanya Shughuli zake kwa Uhuru ........................................ 11

2.5.Kuingilia Bidhaa au Mali ya Mtu Mwingine ........................................ 11

2.6.Kuingilia Ardhi au Shamba lisilo la Kwako ........................................ 11

**3. Uwezo wa Kushitaki** ........................................ **12**

3.1.Kinachozingatiwa Unapotakiwa Kupeleka Shauri Mahakamani ........................................ 12

3.2.Jinsi ya Kufungua Shauri Mahakamani ........................................ 13

3.3.Nafuu anazopata Mtu Baada ya Kushinda Shauri ........................................ 13

**4. Hitimisho** ........................................ **14**

## SHUKRANI

Tunatoa shukrani kwa wanasheria wetu na wale wa kujitolea katika uandaaji wa vijarida hivi. Pia tunawashukuru kwa dhati wale wote walioshiriki kwenye kukirejea kijitabu hiki ili kuandaa toleo hili la nne hususani, Wakili Joanitha Mutayoba, Wakili Theresia Kinabo, Ms. Irene Nambuo na Bw. Rodrick Maro, pamoja na wafanyakazi wote wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu.

# DIBAJI

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kina azma ya kusaidia jamii ya Watanzania kuwa na uwezo wa kufahamu sheria za nchi pamoja na kufahamu haki zao ili kuzilinda na kuzitetea pamoja na kuheshimu haki za wengine ili hatimaye tuwe na jamii yenye utamaduni wa kuheshimu haki za binadamu pamoja na nchi inayoheshimu utawala wa sheria.

Tunafahamu kuwa kwa raia wa kawaida si rahisi kuzifahamu sheria zetu zote, na hata baadhi tu ya sheria zinazomgusa kutokana na mfumo tulio nao, ambao hautoi nafasi kwa watu wote kujua sheria. Hali hii inasababisha watu wengi kujikuta katika matatizo ya kisheria ambayo yangeweza kuepukika kama angejua sheria. Ndiyo maana basi Kituo kimeamua kutoa chapisho hili na mengine, kwa lengo la kutoa msaada wa kisheria kwa raia.

Huu ni usaidizi kisheria unaotoa maelezo mafupi na ya msingi ya kisheria ili kukusaidia ndugu msomaji uweze kupata ufumbuzi au maelezo ya tatizo linalokusibu. Ni lengo letu kuwa, katika kijitabu hiki tunatoa usaidizi wa moja kwa moja kwako wewe pale utakapokuwa na tatizo au mmoja wa ndugu au jamaa zako wanapata matatizo ya

namna hii.

Tunachokuomba ni wewe kusoma kwa makini; na pale suala lako linapokwenda mbali zaidi ya maelezo haya, basi utafute msaada wa kisheria au uende kwa mwanasheria aliye karibu na wewe ili aweze kukusaidia.

Tunaamini utapata usaidizi huu kiurahisi zaidi na maelezo yaliyomo humu yatakusaidia kwa karibu. Umalizapo, tafadhali umsaidie na mwenzako apate usaidizi huu.

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu.

## UTAMBULISHO WA KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu ni shirika binafsi la kujitolea na la hiari ambalo si la kisiaa wala kibiashara. Kituo kimeandikishwa na kusajiliwa kwa mujibu wa Sheria za Tanzania mnamo mwezi Septemba, mwaka 1995. Kabla ya kusajiliwa kama chombo huru, Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kilikuwa ni mradi wa haki za binadamu wa Mfuko wa Kuendeleza Elimu ya Sheria Tanzania (TANLET). Makao makuu ya Kituo ni Dar es Salaam na Arusha kuna ofisi ndogo.

## MAONO

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kina taamali jamii yenye haki na usawa.

## TAMKO LA LENGO MAHUSUSI

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu ni shirika lisilo la kiserikali wala kibiashara linalojibidiisha kukuza uwezo wa jamii ili iweze kukuza, kuendeleza na kulinda haki za binadamu na utawala bora nchini Tanzania.

## LENGO KUU

Lengo kuu la Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu ni kukuza uelewa wa sheria na haki za binadamu kwa jamii kwa ujumla na hasa wale wanajamii ambao kwa sababu moja au nyingine wameachwa nyuma. Uelewa unakuzwa kwa njia ya elimu ya uraia na msaada wa kisheria.

# 1. MAANA YA KUINGILIA KITU KISICHOKUWA CHAKO

Ni pale mtu anapoingia katika eneo/mali ya mtu mwingine bila idhini ya mmiliki wa sehemu/mali hiyo. Kitendo hiki ni kosa na ikibainika hivyo utalazimika kutoka kwenye eneo hilo na kulipa fidia kama mwenye eneo lake atashitaki na ikathibitishwa ulifanya hivyo.

# 2. AINA ZA KUINGILIA KITU KISICHOKUWA CHAKO

**2.1. Kumuingilia/kumbughudhi Mtu bila Idhini Yake**

Kumuingilia mtu bila idhini yake ni kile kitendo cha kumtomasa, kumpiga na/au kumuweka mtu kizuizini kwa makusudi. Kufanya hivyo kuna maana umefanya kosa kwa sababu hukupewa idhini ya kufanya hivyo.

Kuna aina tatu za kuingilia uhuru wa mtu:-

a. Kushambulia kwa maneno;
b. Kutumia nguvu kwa makusudi ili kuumiza;
c. Kumfunga mtu kwa kushindwa kufanya mambo yake kwa uhuru.

### 2.2. Kushambulia kwa Kumtupia Mtu kitu au Kushambulia kwa Maneno

Hii ina maana kwamba pale mtu amemtupia mtu mwingine kitu kiwe chepesi au kizito, awe ametumia nguvu au hajatumia nguvu katika kutupa kitu hicho. Kitendo hicho kinajulikana kama kushambuliwa na ni kosa; kwa sababu kitendo hicho kinaweza kusababisha maumivu au kumkosesha raha au kumweka katika hali ya wasiwasi kwamba anaweza kufanyiwa kitendo ambacho kitamuumiza.

Kushambulia mtu kwa maneno ni pale mtu anapomtukana mwenzake kwa matusi, maneno ya kejeli au kumdhalilisha.

### 2.3. Kutumia nguvu kwa Makusudi kwa Lengo la Kuumiza

Pale mtu anapotumia nguvu kwa lengo la kumuumiza mtu mwingine, nguvu hizi zinaweza kuwa kwa kutumia mikono au kitu kingine; kwa mfano jiwe au chuma. Katika kosa hili, kinachoangaliwa ni kosa lenyewe na sio maumivu ambayo mtu amepata katika kuangalia utendaji wa kosa. Kosa hili likaangukia pande zote mbili jinai na madai.

### 2.4. Kumfunga Mtu Akashindwa Kufanya Shughuli zake kwa Uhuru

Pale ambapo mtu anakuwa hawezi kufanya shughuli zake kwa uhuru kwa kumuogopa mtu mwingine. Ni ile hali ya kumuogopa mtu mpaka akashindwa kwa mfano kupita mtaa fulani, kwenda atakako; kitendo hicho kinakuwa kimemfunga mtu kwa kuwa hana uhuru wa kufanya yale apendayo wakati apendao.

### 2.5. Kuingilia Bidhaa au Mali ya Mtu Mwingine

Kuingilia bidhaa au mali ya mtu mwingine maana yake ni kuingilia mali ya mtu ukiwa unajua unaingilia mali ambayo si yako. Kuingilia huku kunaweza kuwa kushika au kuhamisha mali hiyo. Siyo lazima hasara itokee katika kuingilia mali hiyo, bali tu kile kitendo cha mtu kuingilia mali ya mtu mwingine kwa lengo la kuharibu au kutaka kupekua.

### 2.6. Kuingilia Ardhi au Shamba lisilo la Kwako

Kuingilia ardhi au shamba la mtu mwingine bila ruhusa ya mwenye ardhi au kupewa ruhusa ya kukaa hapo kwa muda fulani, lakini ukazidisha muda huo uliopewa, inaweza kuwa kwa kuweka mali yako, kupanda mazao ya kudumu, kujenga au kuingiza mifugo kwenye ardhi au shamba bila ruhusa ya mwenye shamba.

# 3. UWEZO WA KUSHITAKI

Mtu yeyote anaruhusiwa kushitaki pale ambapo mtu mwingine ameingia kwenye eneo lake bila ruhusa yake. Kikubwa kinachoangaliwa katika kosa hili la kuingilia siyo hasara au uharibifu uliofanywa pale mtu anapoingia katika ardhi, mali au kumuingilia mtu bali kile kitendo chenyewe cha kuingilia bila ruhusa.

## 3.1. Kinachozingatiwa Unapotakiwa Kupeleka Shauri Mahakamani

1. Mtu anayeshitaki lazima awe ndiye mmiliki halali wa ardhi, mali;
2. Mdaiwa awe ameingia kwenye ardhi ya mdai bila ruhusa yake au ameingilia mali ya mdai bila ruhusa ya mdai;
3. Mdaiwa kama alipewa ruhusa ya kuingia

katika eneo la mdai lakini akazidisha muda aliopewa.

### 3.2. Jinsi ya Kufungua Shauri Mahakamani

Pale ambapo mdai ameamua kufungua shauri atatakiwa apeleke hati ya madai katika Mahakama yenye mamlaka ya kuweza kusikiliza shauri hilo, kulingana na thamani ya madai husika:-

a. Mahakama ya Mwanzo ambapo dai la mali inayohamishika ni shilingi 30,000,000/= na 50,000,000/= kwa mali isiyohamishika;
b. Mahakama ya Wilaya au ya Hakimu Mkazi mali isiyohamishika shilingi 200,000,000/= na mali inayohamishika 300,000,000/=;
c. Mahakama Kuu haina kiwango maalum.

Hatua ya pili ni Mahakama ya kutoa taarifa ya kuitwa shaurini (samansi) kwa mdaiwa ambaye anatakiwa kujibu hoja zilizopo ndani ya hati ya madai ndani ya muda unaopangwa na Mahakama kwa mujibu wa sheria.

Baada ya hapo Mahakama itasikiliza shauri hilo.

### 3.3. Nafuu anazopata Mtu Baada ya Kushinda Shauri

a. Kama ni shauri la ardhi, Mahakama itahakikisha kuwa kiwango kitakachotolewa kama fidia ni kile kitakachomwezesha mdai kufanya marekebisho ya ardhi hiyo iwe kama ilivyokuwa kabla ya kuingiliwa;
b. Kama mdaiwa alitengeneza faida kutokana na kutumia ardhi ya mdai, basi mdai akidai atapewa faida hiyo;
c. Nafuu nyingine ni ile ya mdai kwenda Mahakamani kumzuia mdaiwa kuendelea na uharibifu anaoufanya au anaotaka kuufanya.

## 4. HITIMISHO

Ndugu msomaji, tunatumaini kuwa mpaka sasa unafahamu ni nini cha kufanya pale unapoingiliwa uhuru wako ama mali yako.

Tunaomba elimu hii uliyoipata uitoe kwa wengine ili kila mmoja aweze kujua ni nini cha kufanya apatapo tatizo hili.

**KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU**
S. L. P. 75254, Dar es Salaam - Tanzania
**Simu:** +255 22 2773038/48 **Nukushi:** +255 22 2773037
**Barua Pepe:** lhrc@humanrights.or.tz

**DODOMA OFFICE**
Kitalu na 22. Area D,
S.L.P 2289, Dodoma, Tanzania
**Simu/Nukushi:** +255 262350050
**Barua pepe:** lhrc@humanrights.or.tz

**Ofisi ya Arusha**
Barabara ya Olerian, Olosiva Kitalu Na. 116/5,
Sakina kwa Idd, Arumeru
S. L. P. 15243, Arusha - Tanzania
**Simu:** +255 27 2544187
**Barua Pepe:** lhrcarusha@humanrights.or.tz

**Kituo cha Msaada wa Sheria**
Mtaa wa Isere - Kinondoni
S. L. P. 79633, Dar es Salaam - Tanzania
**Simu/Nukushi:** +255 22 2761205/6
**Barua Pepe:** legalaid@humanrights.or.tz

@humanrightstz HakiTV

*Kwa Jamii yenye Haki na Usawa*